

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA TANO

KIKAO CHA NNE

05 APRILI, 2024



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA TANO

KIKAO CHA NNE – TAREHE 05 APRILI, 2024

I. DUA:

II. MASWALI:

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

38. MHESHIMIWA JOSEPH MICHAEL MKUNDI (UKEREWE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, kwa nini ujenzi wa barabara ya Bukiko hadi Bwisya kuitia Katende inayosimamiwa na TARURA haukamiliki kwa zaidi ya miaka miwili sasa.

39. MHESHIMIWA CONSTANTINE JOHN KANYASU (GEITA MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, upi mpango wa Serikali wa kujenga barabara na mitaro Geita Mjini.

40. MHESHIMIWA BENAYA LIUKA KAPINGA (MBINGA VIJIJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Shule za Sekondari Kata za Ngima, Mhongozi na Muungano - Halmashauri ya Mbinga.

41. MHESHIMIWA MUSSA RAMADHANI SIMA (SINGIDA MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itajenga Soko la kisasa Singida Mjini kwani Soko Kuu la Ipembe ni la muda mrefu na miundombinu yake ni chakavu.

OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):

42. MHESHIMIWA PROF. PATRICK ALOIS NDAKIDEMI (MOSHI VIJIJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira):-

Je, kuna ukweli kwamba kina cha maji ya Bahari ya Hindi hapa Tanzania kimeongezeka kutokana na mabadiliko ya Tabianchi na nini athari zake.

WIZARA YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:

43. MHESHIMIWA MOHAMMED JUMAH SOUD (DONGE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki:-

Je, kuna mkakati gani wa kuzihamasisha Balozi za Nchi Mbalimbali Duniani kufungua Ofisi za Ubalozi mdogo Zanzibar.

44. MHESHIMIWA NEEMA KICHIKI LUGANGIRA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki:-

Je, Serikali ipo tayari kuitia utaratibu wa kupima ufanisi wa Balozi zetu wa kuimarisha Diplomasia ya Uchumi kwa kutumia hadidu za rejea zinazofanana.

WIZARA YA AFYA:

- 45. MHESHIMIWA TUNZA ISSA MALAPO (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:-

Je, Hospitali ngapi zinatoa huduma ya tiba ya mionzi kwa Wagonjwa wa Saratani hapa nchini.

WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:

- 46. MHESHIMIWA ERIC JAMES SHIGONGO (BUCHOSA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuendelea kujenga uzio katika sehemu za kuchota maji ili kuzuia vifo vinavyosababishwa na Mamba - Buchosa.

WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

- 47. MHESHIMIWA EMMANUEL PETER CHEREHANI (USHETU):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Kituo cha Polisi katika Halmashauri ya Ushetu.

48. MHESHIMIWA SUMA IKENDA FYANDOMO (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, kwa nini Tanzania hairuhusu Uraia Pacha.

WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:

49. MHESHIMIWA TAMIMA HAJI ABASS (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum:-

Je, Serikali haioni kuwa kutolipwa kwa madeni katika Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake kunaathiri ufanisi wa Mfuko huo.

WIZARA YA KILIMO:

50. MHESHIMIWA FESTO RICHARD SANGA (MAKETE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, Serikali inawahakikisha je Wananchi wa Makete soko na bei ya uhakika ya Zao la Ngano.

WIZARA YA MAJI:

51. MHESHIMIWA KHADIJA SHAABAN TAYA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, lini tatizo la maji Mkoa wa Dodoma litatafutiwa ufumbuzi wa kudumu.

III. HOJA ZA SERIKALI:

WAZIRI MKUU:

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kuitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

(Majadiliano yanaendelea)

**DODOMA
05 APRILI, 2024**

**N.J. MWIHAMBI, *ndc*
KATIBU WA BUNGE**